**KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO KILICHOFANYIKA TAREHE 17/11/2021 KATIKA UKUMBI WA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA MKUNWA**

**WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Thomas Luambano | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) - | Mwenyekiti |
| 2. | Veronica Mwilongo | Afisa Utumishi(W) - | Katibu |
| 3. | Maisha S. Mtipa | Kaimu Mkurugenzi (W) - | Mjumbe |
| 4. | Arthur Mbena | Mwanasheria (W) - | Mjumbe |
| 5. | Epaphroditus C. Sabuni | Afisa Mazingira (W) - | Mjumbe |
| 6. | Gerald B. Sasita | Kaimu DCDO (W) - | Mjumbe |
| 7. | Zuena Myule | Mratibu TASAF (W) - | Mjumbe |
| 8. | Simon Lyimo | Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W) - | Mjumbe |
| 9. | John G. Nkoko | Afisa Ardhi(W) - | Mjumbe |
| 10. | Prisca P. Ntabaye | Afisa Nyuki (W) - | Mjumbe |
| 11. | Isack N. Bilali | Kaimu Afisa Habari(W) - | Mjumbe |
| 12. | Rashidi Niyopa | TEHAMA (W) - | Mjumbe |
| 13. | Dr. Innocent. T.M | Kaimu DLFO (W) - | Mjumbe |
| 14. | Eng. Elias Kuyeko | Kaimu Afisa Ujenzi (W) - | Mjumbe |
| 15. | Patrick J.Almasi | Afisa Ugavi(W) - | Mjumbe |
| 16. | Hassani Dadi | Kaimu Afisa Mipango (W) - | Mjumbe |
| 17. | Scholastica Bernad | Afisa Tarafa - | Mjumbe |
| 18. | Marco Mapunda | Afisa Tarafa - | Mjumbe |
| 19. | Doris Kavindi | Afisa Tarafa - | Mjumbe |
| 20. | Winifrida J. Linyembe | Afisa Tarafa - | Mjumbe |
| 21. | Efenia S. Komba | Kaimu Afisa Kilimo(W) - | Mjumbe |
| 22. | Adamu Shemnga | Afisa Elimu (M) - | Mjumbe |
| 23. | Dr. Matayo Malaika | Kaimu Mganga mkuuu - | Mjumbe |
| 24. | Fadhili S. Mvungi | Afisa Elimu (S) - | Mjumbe |
| 25. | Zuhura Nandala | Kaimu Mwandishi wa Vikao | |

**WASIOHUDHURIA .**

1. Doris Kavindi — Afisa Tarafa - Kitaya Kwa taarifa ya Ugonjwa

**MUH. NA. 61/2021/2022. KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao cha kawaida cha kila mwezi. Alise akidi imetimia alimkaribisha mwenyekiti afungue kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuchangia ajenda kwa ma Baada ya maelezo hayo, alifungua kikao saa 5.20 asubuhi.

Maabara Pia Halmashauri ilipokea fedha Shilingi 250,000,000 kwa ajili ya Ujenzi wa ICU Hospitali ya Nangururwe na Shilingi 90,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba za Watumishi Kituo cha Afya Kilambo

**Hali ya utekelezaji wa mradi**

1. **Kituo cha Afya Mkunwa.**

Kutokana na majengo yaliyopo Kituo cha Afya Mkunwa kuwa ni majengo ya Hospitali ya Wilaya, Halmashauri iliandika barua yenye kumbukumbu namba EA 344/466/05/32 ya tarehe 18/10/2021 kwenda kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuomba kibali cha marekebisho ya matumizi ya fedha za ujenzi. Aidha Mnamo tarehe 8/12/2021 Halmashauri iliandika barua yenye Kumbukumbu namba EA 344/466/05/33 kwenda kwa Katibu tawala Mkoa Kukumbushia maombi ya marekebisho ya matumizi ya fedha.

Mnamo tarehe 11/12/2021 Afisa Mipango Mkoa, Mhandisi Mkoa na timu ya undeshaji wa huduma za Afya Mkoa, Afisa Mipango (W), Mhandisi ujenzi (W) na Mganga Mkuu (W) tulifanya kikao cha Pamoja na kufikia maadhimio yafuatayo:

a) **Fedha za ujenzi zitatumika katika shughuli zifuatazo**
   - Ukamilishaji wa ujenzi wa Jengo la wagonjwa wa nje (OPD)- 205,000,000/=
   - Ujenzi wa kichomea taka (Incinirator)-15,000,000/=
   - Uendelezaji Ujenzi wa Jengo la Maabara-30,000,000/=

b) **Halmashauri itakamilisha shughuli zifuatazo**
   - Kusafisha eneo la Ujenzi
   - Kuchimba Kisima katika eneo la Mradi- Mpaka sasa mawasiliano na Ofisi ya Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini yamefanyika, gharama za kisima ni 27,000,000
   - Ukamilishaji wa Jengo la Mama na Mtoto(Maternity Block)- 230,000,000/= Kutoka kwenye bajeti ya Mwaka wa fedha 2021/2022

2. **Ujenzi wa Jengo la ICU na Nyumba za Watumishi**

Ujenzi wa Majengo haya utatekelezwa kwa kutumia Wakandarasi mpaka kumalizika kwake

**Shughuli zitakazotekezwa na Halmashauri**

- Kuainisha maeneo ambapo miradi hii itatekelezwa
- *Mhandisi wa Halmashauri* kuandaa masterplan inayoonesha eneo ambalo ICU itajengwa, ambapo masterplan imeandaliwa na kuidhinishwa na Mhandisi wa OR-Tamisemi tarehe 17/12/2021
- Kuandaa taratibu za manunuzi ili kupata wakandarasi watakaojenga majengo ya ICU na Nyumba za watumishi. Mnamo tarehe 6/12/2021 tangazo lilitolewa la kutafuta wakandarasi chini ya Bodi ya zabuni.
- Mhandisi wa Halmashauri atakuwa msimamizi mkuu wa mradi huu wakisimamiwa na Mhandisi wa Mkoa.
- Mhandi wa Halmashauri kwa kushirikiana na Mkandarasi atakayeteuliwa wataandaa mpango kazi na ratiba za vikao na kuhakikisha vikao hivyo vinafanyika na taarifa kutumwa Mkoani

**gamoto**

- Eneo lilipendekezwa kujenga Jengo la ICU linakichomea taka hivyo kutakiwa kuondolewa.
- *Kufanya marekebisho* ya walkway ili kupata njia ya kuingia eneo linapojengwa Jengo la ICU

**Mikakati**

- Kujenga kichomea taka kipya cha dharula kwa Shilingi 15,000,000 kutoka kifungu cha ujenzi wa Kituo cha Afya Mkunwa
- Kutengeneza Njia kwenye walkway ili kupata sehemu ya kupita kuingia Jengo la ICU

Baada ya taarifa kuwasilishwa, wajumbe walipokea kisha mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kuchangia na kushauri.

Mjumbe wa kwanza alihoji kama Mkoa tayari waliandika barua ya makubaliano yaliyofanywa kwenye kikao hicho.

Ilijibiwa kuwa bado barua ipo kwa Katibu Tawala Mkoa kwa ajili ya kusainiwa.

Wajumbe waliagiza Mganga Mkuu afuatilie barua kwa Katibu Tawala Mkoa ili kupata maelekezo kuendeleza kituo cha Afya Mkunwa.

Mjumbe mwingine alieleza kuwa kwa vile sehemu ya kujenga ICU ni lazima kuondoa kichome taka. Alihoji tunafanya kwa sababu hatuwezi kujenga ICU bila kuwa na eneo la kuchomea taka.

Aidha waliagiza Afisa Mazingira, Mhandisi wa Ujenzi na Mganga Mkuu wakae pamoja ili kujua eneo sahihi la kujenga kichomea taka bila kuathiri mazingira ya Hospitali.

**b) Taarifa ya Ujenzi wa Madarasa ya UVIKO 19**

Kaimu Mhandisi wa Ujenzi aliwasilisha taarifa ya jumla ya ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19 kwa kuona madarasa yote 54 yapo hatua ya umaliziaji, hata hivyo kwenye ujenzi huo madarasa ya Mangopachanne na Lipwidi kuna changamoto ambazo Halmashauri inatakiwa wafanye marekebisho. Baada ya taarifa kuwasilishwa, wajumbe walipokea kisha mwenyekiti aliongoza michango.

Mjumbe alishauri walimu na walioshiriki katika kufanikisha ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19 wapewe pongezi hata kwa barua. Ushauri ambao ulipokelewa na wajumbe wote. Baada ya michango wajumbe waliagiza afisa utumishi awaandikie Barua za pongezi watu wote waliochangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha ujenzi huo.

**MUHT. NA. 81/2021/2022. KFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kuomba kwenda kuyafanyi kazi mambo yote yaliyoagizwa na kukubaliana kutekelezwa. Baada ya maelezo hay mwenyekiti alifunga kikao saa 7.35 mchana.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA:**

[signature]
**SAINI YA KATIBU**

[signature]
**SAINI YA MWENYEKIT**

13/04/2022
**TAREHE**